JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25











JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

MACHI 2026

# KUHUSU EWURA

## DHAMIRA

Kudhibiti huduma za nishati na maji kwa uwazi, ufanisi na tija ili kuhakikisha ubora, upatikanaji na unafuu wa huduma hizo.

## DIRA

Kuwa mdhibiti wa kiwango cha kimataifa kwa huduma endelevu za nishati na maji.

## MSINGI WA MAADILI YETU

Usawa, Uadilifu, Weledi, Uwajibikaji, Uthabiti na Uwazi

## KAULI MBIU

Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA

# YALIYOMO


UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI ........ v
DIBAJI ........ vi
FASILI YA VIFUPISHO VYA MANENO ........ viii
VIPIMO NA ALAMA ........ ix
FASILI YA VIASHIRIA VYA UTENDAJI ........ x
TASWIRA YA UTENDAJIKAZI WA MAMLAKA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 ........ xii

SEHEMU YA KWANZA ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji ........ 1
1.2 Mchanganuo wa Mamlaka za Maji ........ 2
1.3 Uandaaji wa Taarifa ........ 4

SEHEMU YA PILI ........ 6
2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTENDAJI ........ 6
2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji ........ 6
2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji ........ 7
2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji ........ 8
2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira ........ 10
2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka ........ 10
2.6 Upotevu wa Maji ........ 11
2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji ........ 12
2.8 Utendaji wa Kifedha ........ 14
2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja ........ 17
2.10 Huduma kwa Wateja ........ 17
2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa ........ 18
2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita ........ 20
a. Mamlaka za Maji ........ 20
b. Wizara ya Maji ........ 21
2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji ........ 22
2.14 Uwasilishaji wa Tozo ya Udhibiti ........ 22
2.15 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi ........ 22
2.16 Bodi za Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji ........ 22

SEHEMU YA TATU ........................................................................24
3.0 UPIMAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI ..............24
3.1 Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Maji ..........................24
3.2 Matokeo ya Upimaji ........................................................24

SEHEMU YA NNE ........................................................................31
4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO ..............31

SEHEMU YA TANO ......................................................................36
5.0 HITIMISHO ............................................................................36

# UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mamlaka za Maji) kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

Mamlaka za Maji zina jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za uhakika, salama, na endelevu za maji na usafi wa mazingira. Kutokana na umuhimu huo, EWURA imepewa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti utendaji wa mamlaka hizo ili kuhakikisha malengo haya yanatekelezwa kwa ufanisi.

EWURA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia sekta ya maji, na matokeo yake yanaonekana kupitia uboreshwaji wa huduma mwaka hadi mwaka. Takwimu za utendaji za mwaka huu wa fedha zinaonesha kuimarika zaidi ikilinganishwa na mwaka uliopita, jambo linalothibitisha ukuaji endelevu wa sekta.

Maendeleo chanya katika sekta hii yanaakisi ufanisi wa sera na mikakati ya Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dhamira yake ya kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma imechochea maendeleo makubwa katika upanuzi wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira nchini.

Pamoja na mafanikio hayo, EWURA inaendelea kusisitiza umuhimu wa mamlaka za maji kuongeza kasi katika kupanua na kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira, kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 (Dira 2050). Kupitia Nguzo ya Pili ya Dira 2050 inayohusu Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii, upatikanaji wa majisafi na salama pamoja na huduma bora za usafi wa mazingira umebainishwa kuwa kipaumbele cha kitaifa.

Kwa kuzingatia makadirio kwamba ifikapo mwaka 2050, Tanzania inaweza kukabiliwa na upungufu mkubwa wa maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na athari za mabadiliko ya tabianchi, mamlaka za maji zina wajibu wa kuchukua hatua za kimkakati na endelevu ili kuhakikisha rasilimali za maji zinakuwa endelevu. EWURA itaendelea kuongoza mageuzi ya sekta kupitia udhibiti makini na usimamizi wa kimkakati.

Mwandosya

……………………….

Prof. Mark J. Mwandosya

**Mwenyekiti wa Bodi**

# DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha kwa wadau Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Taarifa hii inatoa tathmini ya kina ya utendaji wa mamlaka za maji, kwa kufanya ulinganisho wa vigezo muhimu baina ya mamlaka za maji, mafanikio, changamoto, pamoja na maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha utendaji. Uchambuzi wa utendaji unaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji zimeendelea kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira ikilinganishwa na miaka iliyopita. Uimarikaji huu umetokana na ushirikiano wa pamoja kati ya mamlaka za maji, Wizara ya Maji, EWURA na wadau wengine wa sekta.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2024/25 ikilinganishwa na 2023/24 ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji kutoka mita za ujazo milioni 736 hadi mita za ujazo milioni 795, sawa na ongezeko la asilimia 8;
(ii) Uzalishaji wa maji uliongezeka kwa asilimia 19 kutoka mita za ujazo milioni 389 hadi mita za ujazo milioni 464;
(iii) Maunganisho ya huduma ya maji kwa wateja yaliongezeka kwa asilimia 9 hadi kufikia 1,812,712 ikilinganishwa na maunganisho 1,669,298;
(iv) Idadi ya wateja wa huduma za majitaka iliongezeka kwa asilimia 4.4, kutoka 56,691 hadi 62,314;
(v) Mamlaka za maji 10 zimeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi na 12 zimepata maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo; na
(vi) Makusanyo ya maduhuli ya mamlaka za maji yameongezeka kwa asilimia 14 kutoka TZS bilioni 419.2 hadi bilioni 479.1.

Pamoja na mafanikio haya, bado baadhi ya maeneo hayaridhishi, nayo ni:
(i) Kuongezeka kwa upotevu wa maji kutoka asilimia 36.8 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi asilimia 42.3 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25;
(ii) Muda wa upatikanaji wa huduma ya maji umeendelea kuwa chini kwa wastani wa saa 14 kwa siku; na

(iii) Mapato ya mamlaka nyingi yameendelea kuwa chini ikilinganishwa na gharama za uendeshaji, na hivyo kushindwa kugharamia kikamilifu shughuli za uendeshaji na matengenezo.

Ili kuendeleza mafanikio huku wakikabiliana na changamoto zilizopo, wadau wa sekta wanapaswa kuongeza juhudi za kupunguza upotevu wa maji kupitia uwekezaji mahsusi katika miundombinu na teknolojia za kisasa. Wadau wanapaswa pia kuboresha uhakika wa huduma kwa kuongeza hatua kwa hatua, muda wa upatikanaji wa maji na kuhakikisha mamlaka za maji zina uwezo wa kugharamia kikamilifu gharama za uendeshaji na matengenezo. EWURA inaendelea kujizatiti kulinda maslahi ya wadau wote wa sekta kwa kuhakikisha usimamizi thabiti wa mamlaka za maji na kuchochea maboresho endelevu, hususan kupitia matumizi ya mifumo ya kidijitali inayolenga kuongeza ufanisi wa taasisi na utoaji wa huduma.

..........................................

Dkt. James A. Mwainyekule

**Mkurugenzi Mkuu**

# FASILI YA VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BOD | Mahitaji ya Oksijeni Kibaiolojia (*Biological Oxygen Demand*) |
| CCC | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (*Consumer Consultative Council*) |
| COD | Mahitaji ya Oksijeni Kikemikali (*Chemical Oxygen Demand*) |
| DAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority*) |
| *E. coli* | Kiashiria cha uchafuzi wa majisafi unaotokana na vimelea *(Escherichia coli)* |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*Energy and Water Utilities Regulatory Authority*) |
| HTM | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni (Handeni Trunk Main) |
| IWA | Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalam wa Maji *(International Water Association)* |
| KASHWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga |
| MajIS | Mfumo wa Uwasilishaji Taarifa za Maji Kielektroniki |
| Mamlaka ya Maji | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira |
| MANAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea |
| RUWASA | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency*) |

# VIPIMO NA ALAMA


| | |
|---|---|
| % | Asilimia |

# FASILI YA VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| i. | Muda wa Ukusanyaji wa madeni | Wastani wa muda katika miezi ambayo wateja huchukua kulipa ankara. Inakokotolewa kwa kuchukua jumla ya madeni ambayo mamlaka ya maji inawadai wateja kutokana na huduma ya majisafi na majitaka kwa mwaka ikigawanywa kwa jumla ya mauzo ya maji na majitaka (ankara) ikizidishwa na miezi 12. Utendaji mzuri ni usiozidi miezi miwili (2) | Miezi |
| ii. | Wastani wa saa za huduma | Saa kwa siku ambazo mtumiaji anaweza kupata maji kwenye bomba lililounganishwa kwenye mtandao wa mamlaka ya maji. Kiwango bora cha huduma ni saa 24 | Saa |
| iii. | Uwiano wa maunganisho ya maji yenye dira | Ni asilimia ya maunganisho ya maji yenye dira za maji zinazofanyakazi. Kiwango kinachotakiwa ni asilimia 100 | Asilimia |
| iv. | Upotevu wa maji | Tofauti ya kiasi cha maji kinachozalishwa au kinachonunuliwa kutoka mamlaka ya maji nyingine na kilichouzwa. Kiwango kinachokubalika cha upotevu wa maji ni chini ya asilimia 20 | Asilimia |
| v. | Uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato | Uwiano wa gharama za uendeshaji kwa mapato, zikijumuisha gharama zote za uendeshaji, uchakavu wa miundombinu pamoja na riba. Usimamizi mzuri wa fedha ni ule wenye uwiano wa chini ya 0.8 | Uwiano |
| vi. | Uwiano wa gharama za watumishi kwa kila mita ya ujazo wa maji yanayozalishwa | Uwiano wa jumla ya gharama za watumishi kwa mita za ujazo wa maji yaliyozalishwa kwa mwaka. | Shilingi/mita za ujazo |
| vii. | Uwiano wa idadi ya watu waliopo kwenye eneo lenye mtandao wa maji | Uwiano wa idadi ya watu waliopo ndani ya mita 200 kutoka kwenye bomba la kusambaza maji dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma | Asilimia |

| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| viii. | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kwenye maunganisho ya majumbani, kwenye magati/vilula na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma. | Asilimia |
| ix. | Ufanisi wa kukusanya mapato | Uwiano wa jumla ya makusanyo kwa jumla ya ankara. Uwiano huu hukokotolewa kwa kugawanya kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha ankara kilichotozwa kikizidishwa kwa 100 | Asilimia |
| x. | Tija ya watumishi | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 ya majisafi na majitaka. Inakokotolewa kwa kugawanya jumla ya watumishi kwa jumla ya maunganisho ya majisafi na majitaka ikizidishwa kwa 1,000. Kiwango kinachofaa ni chini ya watumishi watano kwa kila maunganisho 1,000 | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 |
| xi. | Kukidhi viwango vya ubora wa maji | Uwiano wa sampuli za maji zilizopimwa na kukidhi viwango vya ubora. Hupatikana kwa kugawanya idadi ya sampuli zilizokidhi viwango kwa idadi ya sampuli zilizopimwa na kuzidisha kwa 100. Kiwango kinachofaa ni angalau asilimia 98 | Asilimia |
| xii. | Uwiano wa uendeshaji dhidi ya mapato | Uwiano wa gharama za uendeshaji kwa mapato. Usimamizi mzuri wa fedha ni ule wenye uwiano wa chini ya 0.67 | Uwiano |
| xiii. | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka kwenye maunganisho ya majumbani na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma | Asilimia |
| xiv. | Kukidhi viwango vya ubora wa majitaka | Asilimia ya sampuli za majitaka zilizofikia vipimo vya ubora kulingana na viwango vya ubora vya majitaka vilivyowekwa na shirika la viwango (TBS). Asilimia inayokubalika ni angalau 95 | Asilimia |

# TASWIRA YA UTENDAJAJI KAZI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25



# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilianzishwa kwa Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania kwa lengo la kusimamia shughuli zote za kiuchumi na kiufundi katika sekta za nishati (umeme, mafuta na gesi asilia); na maji (majisafi na usafi wa mazingira).

Majukumu mahususi ya EWURA ni pamoja na kutoa, kuhuisha na kufuta leseni; kuweka na kusimamia viwango vya ubora wa huduma; kudurusu na kusimamia bei za huduma na kutunga sheria ndogo na kanuni. Aidha, EWURA ina jukumu la kufuatilia maendeleo ya sekta zinazodhibitiwa kwa kuzingatia upatikanaji, ubora wa huduma, gharama ya huduma, ufanisi wa uzalishaji, uwekezaji na usambazaji wa huduma; na kusimamia utatuzi wa malalamiko na migogoro.

Taarifa hii inaonesha mwenendo wa jumla wa utendaji wa mamlaka za maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/24. Upimaji wa utendaji wa mamlaka za maji umezingatia mambo muhimu ambayo ni pamoja na namna mamlaka za maji zilivyotoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira na namna zilivyotekeleza malengo yao kama ilivyoainishwa kwenye mipango yao ya biashara.

Muhtasari wa Taarifa hii umegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi wa majukumu ya EWURA, yakiwemo ya usimamizi wa sekta ya maji, mgawanyo wa mamlaka za maji na mbinu za uandaaji wa taarifa. Sehemu ya pili inaelezea kuhusu matokeo ya uchambuzi wa utendaji wa mamlaka za maji. Sehemu ya tatu inaonesha namna ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji unavyofanywa, taratibu zilizotumika na matokeo ya ushindanishaji huo. Sehemu ya Nne ni masuala yaliyobainika, na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kupata ufumbuzi na kuongeza ufanisi katika utendaji wa mamlaka za maji nchini na Sehemu ya tano ni hitimisho la taarifa.

### 1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272, [Sheria ya Maji], kimeipa EWURA jukumu la kudhibiti huduma zinazotolewa na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini. Majukumu hayo ni pamoja na:

a) Kutoa leseni kwa watoa huduma za maji na usafi wa mazingira na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hizo;

b) kutoa miongozo na kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira;

c) kuchambua na kuidhinisha bei za huduma za maji na usafi wa mazingira;

d) kufuatilia ubora wa maji;

e) kukusanya na kuchambua taarifa za utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira;

f) kufanya stadi mbalimbali kwa ajili ya masuala ya kiutawala na kiuendeshaji katika sekta ya maji; na

g) kuandaa taarifa ya mwaka ya utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

Katika kuhakikisha majukumu haya pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika Sheria ya EWURA, Sura 414 yanatekelezwa, na kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 29 (2) cha Sheria ya Maji, EWURA imeandaa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Taarifa hii inalinganisha utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 83 kulingana na vigezo vya utendaji vilivyoainishwa kwenye Muongozo Wa EWURA wa Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi Wa Mazingira wa Mwaka 2022.

## 1.2 Mchanganuo wa Mamlaka za Maji

Kifungu cha 14 cha Sheria ya Maji, kinazitaka mamlaka za maji kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia leseni zinazotolewa na EWURA. Leseni hizo zimegawanywa katika madaraja matatu ambayo ni Daraja la I, Daraja la II na Daraja la III. Mamlaka za maji ambazo hazikidhi vigezo vya kupata madaraja hayo ya leseni hupewa leseni za muda.


Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji za Tanga na Moshi ziliendelea kutoa huduma kwa kutumia leseni za Daraja la I, wakati mamlaka za maji za Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, KASHWASA, Babati, Kahama na Iringa ziliendelea na Leseni za Daraja la II. Kwa upande wa Leseni za Daraja la III, mamlaka za maji 59 zilikuwa zikifanya kazi chini ya daraja hili, huku mamlaka za maji 14, ambazo ni Songe, Busega, Kibondo, Itumba-


Isongole, Loliondo,Utete, MANAWASA, Mkwajuni, Chunya, Namtumbo, Kakonko, Tunduma, Namanyere, na Tunduru zikifanya kazi chini ya Leseni ya Muda.


Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 (1) ya Kanuni za Sheria ya Maji, mamlaka za maji zimepangwa katika madaraja manne, ambayo ni AA, A, B na C kulingana na uwezo wa kifedha na utoaji wa huduma za majisafi.

Vilevile, Mwongozo wa EWURA wa kulinganisha utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022, umeainisha makundi matatu ya mamlaka za maji kulingana na idadi ya wateja ambayo EWURA imetumia kufanya ushindanishaji. Makundi hayo ni pamoja na Kundi la I kwa Mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000, Kundi la II - Mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na Kundi la III - Mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000.

Mchoro Na. 1, unaonesha Madaraja ya leseni, Madaraja ya Mamlaka za Maji na Makundi ya Mamlaka za Maji kulingana na uwezo wa utoaji huduma.



**Mchoro Na. 1: Madaraja ya Leseni, Madaraja ya Mamlaka na Kundi**

**Fasili ya Madaraja ya Leseni**

| | |
|---|---|
| **Daraja la I** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na uwezo wa kurejesha gharama zote za uendeshaji |
| **Daraja la II** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na uwezo wa kurejesha gharama za uendeshaji isipokuwa sehemu ya gharama za uwekezaji |
| **Daraja la III** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye bado anasaidiwa na Serikali kifedha, kiuendeshaji na kiufundi na ana uwezo wa kurejesha kiasi cha gharama zake za uendeshaji |
| **Leseni ya Muda** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye hajakidhi vigezo vya kupata leseni ya Daraja la I, II au III (mwenye miundombinu na rasilimali watu kwa ajili ya utoaji wa huduma) |

**Fasili ya Madaraja ya Mamlaka za Maji**

| | |
|---|---|
| **AA** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wake na zinamudu gharama za uendeshaji, matengenezo, uchakavu, na zinaweza kurudisha gharama za uwekezaji |
| **A** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 75 ya wakazi wake na zinamudu gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uchakavu |
| **B** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 65 na zinamudu gharama zote za uendeshaji na matengenezo |
| **C** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji chini ya asilimia 65 na zinamudu gharama za uendeshaji na matengenezo isipokuwa sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo inagharamiwa na Serikali |

## 1.3 Uandaaji wa Taarifa

Uandaaji wa taarifa hii ulihusisha ukusanyaji, uchambuzi, na uhakiki wa

taarifa za kiufundi, kibiashara, na kifedha kutoka mamlaka za maji. Vyanzo vikuu vya takwimu hizo vilijumuisha mfumo wa kielektroniki wa uwasilishaji wa taarifa za Mamlaka za Maji (MajIS), na mfumo wa NSMIS wa uwasilishaji wa taarifa za usafi wa mazingira, taarifa za utendaji za mwaka, taarifa za fedha, na mipango ya biashara iliyowasilishwa na mamlaka husika.


Ili kuhakikisha usahihi na uhakika wa takwimu na taarifa zilizowasilishwa, hatua mbalimbali zilitekelezwa, ikiwemo kuzikagua mamlaka za maji, kuomba ufafanuzi pale ambapo takwimu zilionesha mwenendo usio wa kawaida ikilinganishwa na taarifa za awali, au pale ambapo takwimu au maelezo yalikuwa yanakinzana au yasiyo sahihi. EWURA pia ilifanya mikutano na watendaji wakuu wa mamlaka za maji ili kujadili na kuthibitisha taarifa na takwimu zilizopokelewa kabla ya kuchapishwa. Mikutano hiyo pia ilihudhuriwa na watendaji kutoka Wizara ya Maji na Wizara ya Afya. Aidha, EWURA ilifanya mikutano ya mashauriano na Wizara hizo ili kujadili rasimu ya taarifa.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTENDAJI

Uchambuzi wa kiufundi, kifedha na utendaji wa mamlaka za maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 umefanyika kwa kulinganisha utendaji wa Mwaka wa Fedha 2023/24 na kuonesha matokeo yafuatayo:

### 2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji




Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mahitaji ya maji yaliongezeka kwa asilimia 4.5, uwezo wa miundombinu ya uzalishaji wa maji kwa asilimia 8 na uzalishaji maji kwa asilimia 19.3 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/24. Licha ya ongezeko hili, uzalishaji wa maji ulitosheleza asilimia 52 tu ya mahitaji ya maji kwa maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji. Ongezeko la mahitaji ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji linatokana na ukuaji wa idadi ya watu pamoja na kutanuka kwa maeneo ya huduma ya mamlaka za maji.


Uchambuzi wa uwiano wa uzalishaji dhidi ya uwezo wa mitambo ya uzalishaji maji, unaonesha ongezeko la hadi asilimia 58 katika Mwaka wa Fedha 2024/25 kutoka asilimia 53 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa matumizi ya miundombinu iliyopo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za maji.

Katika kipindi cha taarifa, uwiano wa mahitaji ya maji dhidi ya uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji ulikuwa asilimia 89. Hii inaonesha kuwa, miundombinu iliyopo hata ikitumika kikamilifu, haiwezi kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji, hivyo kuna haja ya kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji maji.

## 2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji

### a. Upatikanaji wa huduma ya maji

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, uwiano wa idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo yenye mtandao wa maji uliendelea kuwa asilimia 84 kama ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, ikimaanisha kuwa upanuzi wa mtandao umeenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu.




Vilevile, uwiano wa watu wanaopata huduma ya maji ulishuka kutoka asilimia 66 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi asilimia 64 katika Mwaka wa Fedha 2024/25. Kushuka kwa asilimia ya watu wanaopata huduma ya maji kunatokana na kasi ndogo ya kuunganisha wateja wapya ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa:


i) Mamlaka ya maji Maswa ilikuwa na ongezeko la asilimia 24 la uwiano wa watu wanaopata huduma ya maji;

ii) Mamlaka za maji Igunga, Songea, na Nzega, zilifikia uwiano wa zaidi ya asilimia 90 ya idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kwenye mtandao; na

iii) Mamlaka za maji za Ushirombo, Mugango-Kiabakari, Vwawa-Mlowo, Geita, Kilindoni, na Tunduma zilikuwa na uwiano wa chini wa zaidi ya asilimia 20 wa watu wanaopata huduma ya maji;

iv) Mamlaka za maji za Igunga, Nzega, Songea, Sengerema, Sumbawanga, Same-Mwanga, Iringa, DAWASA, Wanging'ombe, Tanga, Kigoma, Makambako, Arusha, Moshi, Lushoto, na Mbeya zilifikia angalau asilimia 90 ya wanaoishi ndani ya mtandao wa maji.

b. **Muda wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji**





Wastani wa muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa siku kwa maeneo ya huduma ya mamlaka za maji umeendelea kuwa saa 14, ambao ni chini ya kiwango kinachotakiwa cha saa 24.

Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji ambazo zilikuwa na wastani wa muda wa upatikanaji wa maji unaotakiwa wa saa 24 ni pamoja na Iringa, Moshi, Songea, Igunga, na Nzega. Mamlaka za maji za Itumba-Isongole, Kondoa, Liwale, Ngara, Songe, na Mkwajuni zilikuwa na wastani wa muda wa upatikanaji wa maji usiozidi saa tano kwa siku.

## 2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji

a. **Miundombinu ya Kusafisha na Kutibu Maji**




Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, asilimia 100 ya mamlaka za maji zilikuwa na miundombinu ya kusafisha na kutibu maji ikilinganishwa na asilimia 97.6 katika Mwaka wa Fedha 2023/24.


Kati ya hizo:

i) Mamlaka za maji 36 zilisafisha na kutibu maji kwa kutumia mitambo ya kisasa;

ii) Mamlaka za maji 47 zilisafisha na kutibu maji kwa kutumia dawa za kuua vimelea vya magonjwa;

iii) Kati ya mamlaka hizo 47, 23 zinahitaji kusafisha na kutibu maji kwa njia za kisasa zaidi ili kukidhi matakwa ya viwango ya ubora vinavyotakiwa. Mamlaka hizo ni pamoja na Kondoa, Kyela-Kasumulu, Liwale, Ludewa, Lushoto, Mafinga, Makambako, Makete, Mbinga, Mbulu na Mkwajuni. Nyingine ni Mpanda, Mpwapwa, Namanyere, Namtumbo, Ngara, Njombe, Rombo, Rujewa, Tukuyu, Turiani, Vwawa-Mlowo, na Wanging'ombe.

**b. Ubora wa Maji**





Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, ubora wa maji uliimarika kwa asilimia 9, 5 na 1 kwa viashiria vya vimelea vya magonjwa (*E. coli),* tope (turbidity) na kiwango cha dawa ya kuua vimelea vya magonjwa *(residual chlorine)* mtawalia, wakati kiwango cha asidi (pH) kilishuka kwa asilimia 5 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Pamoja na kuimarika huko, kwa ujumla, kiwango cha viashiria vya vimelea vya magonjwa *(E. coli)*, kiwango cha tope (turbidity), kiwango cha dawa ya kuua vimelea *(residual chlorine)* na kiwango cha asidi (pH) vimefikia asilimia 97,77, 27 na 81, mtawalia ambayo ni chini ya kiwango cha asilimia 100 kinachotakiwa. Kutokukidhi huko kulitokana zaidi na upungufu wa watumishi wenye sifa wa kusimamia ubora wa maji, pamoja na miundombinu ya kutibu maji isiyotosheleza.

## 2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira

### a. Mtandao wa Mabomba ya Majitaka




Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 mamlaka 11 za maji ziliendelea kutoa huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao wa mabomba kama ilivyokuwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Mamlaka hizo ni Arusha, DAWASA, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Tabora, na Tanga.

Kupitia mamlaka hizo, idadi ya wateja wanaopata huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao wa bomba ya majitaka iliongezeka kutoka wateja 56,691 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi 62,314 Mwaka wa Fedha 2024/25. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na uhamasishaji wa jamii zilizo karibu na mtandao wa majitaka kuunganishwa na mitandao hiyo.

Kwa upande wa uwiano wa idadi ya watu wanaoishi katika eneo lenye mtandao wa majitaka katika mamlaka hizo, uwiano umeongezeka kutoka asilimia 5.61 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi kufikia asilimia 5.71 Mwaka 2024/25.

## 2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka

### a. Miundombinu ya Kutibu Majitaka na Topekinyesi

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji 24 kati ya 83 zilikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi ikilinganishwa na mamlaka za maji 23 zilizoripotiwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuanza kufanya kazi kwa miundombinu ya mamlaka ya maji Tanga katika eneo la Muheza na Pangani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa:


i) Mamlaka 10 za maji ambazo ni Babati, Bunda, Chato, DAWASA, Igunga, Mpanda, Musoma, Njombe, Singida, na Tabora zimeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi; aidha, ujenzi unaofanywa na mamlaka za DAWASA na Tabora ni kwaajili ya kuongeza huduma ili kuendana na mahitaji.

ii) Mamlaka 12 za maji za Bukoba, Gairo, Kondoa, Ludewa, Mafinga, Makete, Makonde, Manyoni, MANAWASA, Mtwara, Namanyere, na Tanga zimeshapata maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi. Mamlaka za Tanga na Bukoba ardhi iliyopatikana ni kwa ajili ya kuongeza ujenzi wa miundombinu.

iii) Mamlaka 41 za maji hazikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi wala eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

### b. Ubora wa Majitaka


Kiwango cha ubora wa majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira kimeongezeka kutoka asilimia 33 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi asilimia 43 Mwaka wa Fedha 2024/25, kuimarika huo kumetokana na ukarabati wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi.




## 2.6 Upotevu wa Maji

Kiwango cha upotevu wa maji kimeongezeka na kufikia asilimia 42.3 katika Mwaka wa Fedha 2024/25 kutoka asilimia 36.8 kwa mwaka uliopita. Kiwango hiki ni sawa na upotevu wa mapato yenye thamani ya shilingi bilioni

182.6, ikilinganishwa na kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika kisichozidi asilimia 20. Upotevu huu wa maji kwa kiasi kikubwa umechangiwa na kutokuwepo kwa dhamira ya dhati miongoni mwa mamlaka za maji ya kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu huo.




Katika mwaka wa mapitio, yafuatayo yamebainika: -

i) Mamlaka za maji za Nzega, Biharamulo, Mwanhuzi, Maganzo, KASHWASA, Busega, na Shinyanga zilikuwa na upotevu wa maji usiozidi asilimia 20;

ii) Mamlaka za maji za Mugango-Kiabakari, Same-Mwanga, Rombo, Namanyere, Mbulu, HTM, DAWASA na Mkwajuni zilikuwa na upotevu wa maji wa zaidi ya asilimia 50; na

iii) Mamlaka za maji za Ifakara, Kasulu, Liwale, Mpanda, na Bariadi ziliimarika na kupunguza upotevu wa maji kwa zaidi ya asilimia 10 ikilinganishwa na Mwaka uliopita.

## 2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji

Katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji kwa mamlaka za maji, EWURA iliandaa miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021 ambao unazitaka mamlaka za maji kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa; na

(ii) Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima na Kufanyia Matengenezo Dira za Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021, ambao unazitaka mamlaka za maji kuwa na sera ya dira za maji na kanzidata.

Uchambuzi umefanyika ili kuona ni kwa kiasi gani mamlaka za maji zinafanya jitihada za kudhibiti upotevu huo ili usizidi kiwango kinachokubaliwa. Viashiria vilivyofanyiwa uchambuzi ni kama ifuatavyo: -

**a. Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji**

Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021 unazitaka Mamlaka za maji kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji. Aidha, Mwongozo huo unasisitiza umuhimu wa mamlaka za maji kuandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji kwa mujibu wa mwongozo wa Jumuiya ya Kimataifa ya MajI (IWA) ili kujua maeneo yenye upotevu wa maji kwenye mamlaka zao. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji 28 kati ya 83 zilikuwa na mikakati iliyoidhinishwa ya kupunguza upotevu wa maji ikilinganishwa na mamlaka za maji 25 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Mamlaka hizo ni Arusha, DAWASA, Dodoma, Iringa, Kahama, Moshi, Musoma, Shinyanga, Songea, Tanga, Bukoba, Babati, Bariadi, na KASHWASA. Nyingine ni Makonde, Maswa, Biharamulo, Bunda, Gairo, Igunga, Karatu, Mbinga, Mbulu, Ngara, Nzega, Same–Mwanga, Utete, na Busega. Aidha, mamlaka zote 83 za maji ziliandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji.

**b. Sera ya Dira za Maji**

Sera ya Dira ya Maji inalenga kuweka mfumo wa usimamizi wa dira za maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji pamoja na kuweka utaratibu wa ufungaji wa dira za maji kwa wateja ili kudhibiti upotevu wa maji. Uchambuzi unaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka 37 za maji kati ya 83 zilikuwa na sera za dira za maji zilizoidhinishwa ikilinganishwa na mamlaka 31 za maji Mwaka wa Fedha 2023/24. Mamlaka hizo ni Arusha, DAWASA, Dodoma, Iringa, Kahama, Moshi, Musoma, Mwanza, Shinyanga, Songea, Tabora, Tanga, Bukoba, Kigoma, Babati, Bariadi na Geita. Nyingine ni Vwawa–Mlowo, KASHWASA, Makonde, MANAWASA, Maswa, Biharamulo, Bunda, Igunga, Karatu, Manyoni, Mbinga, Mbulu, Mpwapwa, Ngara, Nzega, Ruangwa, Ushirombo, Utete, Busega, na Mkwajuni.

**c. Kanzidata ya Dira za Maji**

Katika kudhibiti upotevu wa Maji, Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima na kufanyia matengenezo dira za maji kwa Mamlaka za Maji

wa Mwaka 2021 unazitaka mamlaka za maji kuwa na Kanzidata ya Dira za Maji. Kanzidata inawezesha mamlaka za maji kutunza kumbukumbu muhimu za dira za maji na hivyo kuwezesha usimamizi na matenegenezo yake. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka 42 za maji kati ya 83 zilikuwa na kanzidata ya dira za maji ikilinganishwa na mamlaka 6 za maji katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

**d. Uhakiki wa Dira za Maji**

Mamlaka za maji zinatakiwa kuhakiki dira za maji zinazotumika ili kubaini usahihi wake katika kupima matumizi ya maji ya wateja. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji 6 kati ya 83 ambazo ni Iringa, Mbeya, Songea, Ifakara, Nzega, na Turiani zilihakiki upya dira hizo.

**e. Uwiano wa Maunganisho yenye Dira za Maji**


Uwiano wa maunganisho ya maji yenye dira umepungua kwa asilimia 1.1 katika Mwaka wa Fedha 2024/25 na kufikia asilimia 94 kutoka asilimia 95 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha huduma kinachokubalika cha asilimia 100.

Mamlaka 62 za maji kati ya 83 zilikuwa na uwiano wa asilimia 100 wa maunganisho kwa wateja yenye dira za maji. Mamlaka za maji za Kasulu, Ludewa, na Namtumbo zilikuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 20 katika uwiano wa maunganisho yenye dira za maji. Mamlaka ya maji ya Kyela-Kasumulu ilikuwa na uwiano mdogo wa asilimia 1 kutokana na maji yanayozalishwa kuwa na tope jingi hususan kipindi cha mvua na hivyo kusababisha mita kuziba kama ilivyokuwa katika mwaka wa fedha uliopita.

## 2.8 Utendaji wa Kifedha

**a. Ukusanyaji na uzalishaji wa Mapato**

Makusanyo ya mapato kwa Mamlaka za Maji yaliongezeka kwa asilimia 14 katika Mwaka wa Fedha 2024/25 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 7 katika Mwaka wa Fedha 2023/24.




Hii inatokana na kuongezeka kwa ankara za mauzo ya maji na mapato yatokanayo na shughuli nyingine, hususan uunganishaji wa wateja wapya.

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mapato ya uendeshaji ya mamlaka za maji yaliongezeka hadi kufikia Shilingi milioni 490,253, kutoka Shilingi milioni 442,440 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 11 kwa mwaka. Ongezeko hili linaashiria kuimarika kwa uwezo wa kuzalisha mapato pamoja na uboreshaji wa utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya huduma ya kila Mamlaka.

Mamlaka ya maji DAWASA imeendelea kuwa mamlaka yenye mapato makubwa zaidi ikiwa na mapato ya shilingi milioni 159,249, sawa na asilimia 32 ya mapato yote yaliyokusanywa na mamlaka za maji katika Mwaka wa Fedha 2024/25. Kiwango hiki kinatokana na kuwa na wigo mpana wa wateja ikilinganishwa na mamlaka nyingine. Aidha, mamlaka ya maji ya Kilindoni iliendelea kuwa na mapato madogo zaidi ambayo ni shilingi milioni 40.6 katika Mwaka wa Fedha 2024/25, ikipungua kutoka shilingi milioni 44.5 zilizorekodiwa katika mwaka wa fedha uliopita.

## b. Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato





Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, ufanisi wa mamlaka za maji katika ukusanyaji wa mapato uliimarika na kufikia wastani wa asilimia 92.2, kutoka asilimia 91.9 uliofikiwa kipindi kilichopita. Ongezeko hili linaakisi kuimarika kwa mtiririko wa fedha kwa mamlaka, jambo linaloimarisha uthabiti wa kifedha na uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Pamoja na kuimarika huku, ufanisi wa jumla katika ukusanyaji wa mapato uliendelea kuwa chini ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 95. Mamlaka 41 za maji zilishindwa kufikia kiwango cha


ufanisi kinachokubalika cha asilimia 95, Gairo ikiwa ni mamlaka ya maji yenye ufanisi wa chini kabisa wa asilimia 61.

## c. Bei za Maji




Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, bei za maji ziliongezeka kufikia wastani wa shilingi 1,462 kwa mita ya ujazo kutoka shilingi 1,437 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Ongezeko hili limetokana kutumika kwa bei mpya za maji zilizoidhinishwa katika miaka iliyotangulia. Kwa ujumla, wastani wa bei za maji ulikuwa kati ya shilingi 300 hadi 3,590 kwa mita za ujazo. Utofauti wa bei kwa kila mamlaka ulitokana na tofauti ya mazingira ya uendeshaji. Mamlaka za maji zilizoanza kutumia bei mpya ni Arusha, Moshi, Mbeya, Songea, Sumbawanga, Babati, Lindi, Bariadi, Makonde, Lushoto, Mafinga, Mpwapwa, na Mbulu.

## d. Uwiano wa Mapato na Gharama za Uendeshaji





Katika Mwaka wa mapitio, wastani wa uwiano wa uendeshaji (working ratio) wa mamlaka za maji ulikuwa 1.3 kama ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, ikiashiria kuwa uzalishaji wa mapato na gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa kiwango kinachokaribiana katika kipindi husika.

Kwa upande wa uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu wa miundombinu dhidi ya mapato (operating ratio), uchambuzi unaonesha uliimarika hadi kufikia uwiano wa 1.95 ikilinganishwa na uwiano wa 2.97 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Kupungua kwa uwiano huo kunaashiria kuimarika kwa uwezo wa mamlaka za maji kugharamia uendeshaji, ikiwemo gharama za uchakavu wa miundombinu. Pamoja na kuimarika huko, viwango hivi bado vipo juu ya viwango vinavyokubalika vya 0.67 na 0.80.

Mamlaka ya maji Tunduru ilikuwa na uwiano wa 0.5 wa gharama za uendeshaji na uchakavu wa miundombinu dhidi ya mapato wakati mamlaka ya maji ya Same – Mwanga ikiwa na uwiano wa juu wa 14.6 unaohusishwa na utekelezaji wa mradi wake mkubwa wa maji.

## 2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja




Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, idadi ya watumishi wa mamlaka za maji iliongezeka na kufikia watumishi 6,897 ikilinganishwa na watumishi 6,837 katika mwaka wa fedha uliopita. Pamoja na ongezeko hili, uwiano wa watumishi kwa idadi ya wateja 1,000 wa majisafi na majitaka uliimarika na kufikia 3.7 ikilinganishwa na 4.0 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Utendaji huu upo ndani ya kiwango kinachokubalika cha chini ya watumishi 5 kwa kila wateja 1,000. Uchambuzi unaonesha kuwa, mamlaka 50 za maji zilikidhi kiwango hiki cha uwiano ikilinganishwa na mamlaka 24 katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

## 2.10 Huduma kwa Wateja

Katika kuimarisha huduma kwa wateja, Mamlaka za Maji zinapaswa kuwa na Mikataba ya Huduma kwa wateja, pamoja kupokea na kushughulikia malalamiko yao. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, uchambuzi wa vigezo hivi unaonesha yafuatayo;

a. Mamlaka za maji 73 sawa na asilimia 88 zilikuwa na Mikataba ya Huduma kwa wateja iliyoidhinishwa, wakati Shinyanga, Kigoma,

Maswa, Wanging'ombe, Kondoa, Lushoto, Mafinga, Tukuyu, Maganzo, na Mkwajuni zikiwa kwenye mchakato wa kuandaa mikataba hiyo.

b. Malalamiko 463,740 yalipokelewa na kati ya hayo, asilimia 58.6 yalihusu mivujo na msukumo, asilimia 12.6 yalihusuhu majitaka, asilimia 11.5 yalihusu ankara na dira za maji, asilimia 4.5 yalihusu maunganisho ya maji na asilimia 12.8 yalihusu mambo mengineyo.

c. Malalamiko 306,156 sawa na asilimia 66 yalitatuliwa kikamilifu ikilinganishwa na asilimia 61 katika mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, kati ya malalamiko hayo yaliyotatuliwa, asilimia 82 yalitatuliwa ndani ya siku tano za kazi kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Maji na Usafi wa Mazingira (Leseni na Ubora wa Huduma) za Mwaka 2020.

Kwa ujumla, uchambuzi unaonesha kuwa kumekuwa na maboresho katika kushughulikia na utoaji wa huduma kwa wateja. Hata hivyo, maendeleo zaidi yatategemea uimarishaji wa mifumo ya ufuatiliaji wa malalamiko kwa wakati, upatikanaji wa rasilimali na watumishi wa kutosha katika vitengo vya huduma kwa wateja, pamoja na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji kupitia ukaguzi wa utendaji na tathmini za mrejesho wa wateja.

## 2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa

### a. Uwasilishaji wa Mipango ya Biashara na Programu za Ufuatiliaji wa Ubora wa Majisafi na Majitaka

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka 53 za maji kati ya 83 zilikuwa na mipango ya biashara. Mamlaka za maji ambazo hazikuwa na mipango ya biashara ni pamoja na DAWASA, Mtwara, Musoma, Bariadi, HTM, KASHWASA, Maswa, Mugango–Kiabakari, Bunda, Chato, Chunya, Itumba–Isongole, Kilindoni, Kilwa Masoko, Kiomboi, Kondoa, Kyela–Kasumulu, Liwale, Mwanhuzi, na Namanyere.

Nyingine ni Namtumbo, Ruangwa, Same–Mwanga, Sengerema, Tunduru, Ushirombo, Tunduma, Busega, Mkwajuni, na Kakonko. Aidha, kwa upande wa Programu za Ufuatiliaji wa Ubora wa Majisafi na Majitaka, mamlaka 81 za maji kati ya 83 zilikuwa na programu hizo, isipokuwa mamlaka za Kakonko na Mkwajuni ambazo hazikuwa nazo.

## b. Uwasilishaji wa Taarifa

Mamlaka za maji zinapaswa kuwasilisha taarifa za kila mwezi za kielektroniki (MajIS), taarifa za mwaka za kiufundi na za kifedha, na taarifa za mwaka za MajIS. Takwimu zinaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, uwasilishaji wa taarifa hizo ulikuwa ni asilimia 74, 75, 84, na 100 mtawalia ikilinganishwa na asilimia 68,72,77, na 95 katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Mchanganuo wa uwasilishaji wa taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

i. Mamlaka 19 za maji za Arusha, Dodoma, Moshi, Musoma, Mwanza, Songea, Tanga, Sumbawanga, Lindi, Bariadi, Makonde, Igunga, Itumba-Isongole, Karatu, Kishapu, Ludewa, Nzega, Tunduma, na Turiani ziliwasilisha taarifa za kiufundi na kifedha kwa wakati;

ii. Mamlaka 21 za Arusha, Dodoma, Moshi, Musoma, Mwanza, Songea, Tanga, Sumbawanga, Lindi, Bariadi, Makonde, Biharamulo, Igunga, Itumba-Isongole, Karatu, Kishapu, Ludewa, Makete, Nzega, Tunduma, na Turiani ziliwasilisha taarifa za kila mwezi za kielektroniki (MajIS) kwa wakati. Kwa miaka mitatu mfululizo, mamlaka za maji za Songea na Nzega ziliwasilisha taarifa za kila mwezi za kielektroniki (MajIS) kwa wakati;

iii. Mamlaka zote 83 ziliwasilisha taarifa za mwaka za kielektroniki (MajIS) kwa wakati;

iv. Mamlaka 62 ziliwasilisha taarifa za mwaka za kiufundi kwa wakati, wakati 13 zikiwasilisha kwa kuchelewa na 8 hazikuwasilisha kabisa.

v. Kwa miaka mitatu mfululizo, mamlaka za maji za Dodoma, Iringa, Moshi, Musoma, Mwanza, Songea, Tabora, Tanga, Singida, Babati, Lindi, Njombe, Makonde, Chunya, Igunga, Itumba-Isongole, Kishapu, Liwale, Loliondo, Ludewa, Mpwapwa, Namtumbo, Nzega, Rujewa, Maganzo na Makambako zimekuwa zikiwasilisha taarifa zao za kiufundi za mwaka kwa wakati

vi. Mamlaka za maji 70 ziliwasilisha taarifa za kifedha kwa wakati, 11 kwa kuchelewa na 2 hazikuwasilisha kabisa. Kwa miaka mitatu mfululizo mamlaka za maji za Dodoma, Morogoro, Moshi, Musoma, Mwanza, Shinyanga, Songea, Bukoba, Singida, Sumbawanga, Geita, Njombe, Mugango-Kiabakari, Chunya,

Kasulu, Kishapu, Ludewa, Makete, Manyoni na Namtumbo ziliwasilisha taarifa hizo kwa wakati.

## 2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita

Katika kuhakikisha changamoto za tathmini ya utendaji zilizobainishwa kwenye Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, EWURA ilitoa jumla ya mapendekezo 14 kwa ajili ya kufanyiwa kazi na mamlaka za maji. Kati ya hayo, pendekezo moja utekelezaji wake unakamilika Juni 2030, tisa kufikia Juni 2026, na manne ni endelevu. Aidha, manne yalikuwa ni maoni na ushauri uliolekezwa kwa Wizara ya Maji kwa ajili ya kuzingatiwa. Kwa ujumla, utekelezaji wa mapendekezo hayo pamoja na maoni na ushauri unaendelea kufanyiwa kazi na tathmini yake inatarajiwa kuanza kutolewa taarifa ifikapo mwezi Juni 2026 kulingana na muda wa utekelezaji ulivyoainishwa.

Mapendekezo na Ushauri ulitolewa kwa Mamlaka za Maji na Wizara ya Maji ni kama ifuatavyo

**a. Mamlaka za Maji**

Mapendekezo na ushauri kwa Mamlaka za maji ilikuwa:

i) Mamlaka za maji ziimarishe ubora wa maji kwa kuandaa na kutekeleza Mwongozo wa utaratibu wa kutibu maji (Standard Operating Procedures);

ii) Mamlaka za Maji ziwe na vifaa vya kupima kiwango cha dawa, ubora wa maji kwa ajili ya kufuatilia vigezo mbalimbali vya ubora ikiwamo kiwango cha dawa na vimelea vya magonjwa;

iii) Mamlaka zitibu maji kwa kutumia wataalam wenye sifa stahiki;

iv) Mamlaka za maji ziongeze uwezo wa miundombinu ya kutibu majitaka iliyopo au kujenga miundombinu ya ziada, au mipya ili kukidhi mahitaji ya kutibu maji;

v) Mamlaka za maji zifanye ukarabati wa miundombinu ya kutibu majitaka mara kwa mara ili kuleta ufanisi;

vi) Mamlaka za maji ziweke mikakati ya kufikia asilimia 95 ya mtandao wa maji katika Mipango yao ya Biashara ikiwa ni pamoja na kuingia ubia na sekta binafsi ili kukabiliana na changamoto ya huduma ya maji isiyotosheleza;

vii) Mamlaka za maji zihakikishe wateja wapya wanaunganishiwa huduma ya maji kwa wakati ili kutekeleza kikamilifu Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

viii) Mamlaka za maji ziandae na kutekeleza mkakati wa kupunguza upotevu wa maji;

ix) Mamlaka za maji ziainishe kwenye Mipango ya Biashara mikakati ya kupata eneo la kujenga miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi;

x) Mamlaka za maji zishirikishe Sekta binafsi kwenye ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi;

xi) Mamlaka za maji ziongeze mtandao wa usambazaji maji, uwezo wa miundombinu iliyopo ya uzalishaji na idadi ya wateja ili kukidhi mahitaji;

xii) Mamlaka za maji zitoe kipaumbele kwa maandalizi ya mipango ya biashara inayoakisi gharama halisi za uendeshaji zitakazojumuishwa kwenye marekebisho ya bei mpya za maji ili kupata bei zinazowezesha kurejesha gharama za uendeshaji;

xiii) Mamlaka za maji zibuni na kutekeleza programu jumuishi za usafi wa mazingira ili kukabiliana na changamoto ya huduma za usafi wa mazingira zisizotosheleza ikiwemo mtandao mdogo wa majitaka; na

xiv) Mamlaka za maji zitekeleze Mwongozo wa EWURA wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na topekinyesi kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2020.

**b. Wizara ya Maji**

i) Kufuatia changamoto ya wastani mdogo wa kukidhi kiwango cha ubora wa maji, Wizara ya Maji iwezeshe mamlaka za maji kujenga miundombinu ya kutibu maji;

ii) Wizara ya Maji iziwezeshe mamlaka za maji kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi kwakuwa mamlaka za maji 52 hazina miundombinu hiyo; na

iii) Wadau wakuu katika mchakato wa marekebisho ya bei za maji wazingatie sheria zilizopo.

## 2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji 16 za Mpwapwa, Dodoma, Mafinga, Mtwara, Makonde, Lindi, Bariadi, Moshi, Mbulu, Babati, Arusha, Lushoto, Orkesumet, Songea, Mbeya na Sumbawanga ziliidhinishiwa bei mpya za huduma zilizo ambatana na masharti ya kutekeleza. Kwa ujumla, utekelezaji wa masharti ya bei za maji umeongezeka na kufikia asilimia 64 ikilinganishwa na asilimia 61 iliyofikiwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

## 2.14 Uwasilishaji wa Tozo ya Udhibiti

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, EWURA ilipokea kiasi cha shilingi 4,588,190,810.93 sawa na asilimia 47.46 ya kiasi cha Shilingi 9,666,575,101.20 kilichopaswa kuwasilishwa na mamlaka za maji kama tozo. Uchambuzi wa uwasilishaji wa tozo ya udhibiti unaonesha yafuatayo: -

i. Mamlaka 27 za maji ambazo ni Iringa, Kahama, Moshi, Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Singida, Mpanda, Njombe, Babati, KASHWASA, Biharamulo, Igunga, Kibondo, Kilindoni, Kishapu, Loliondo, Ludewa, Lushoto, Manyoni, Nzega, Songe, Tukuyu, Maganzo, Tunduma, Turiani na Kakonko, ziliwasilisha tozo yote iliyoainishwa kwenye ankara**;**

ii. Mamlaka nane za maji za DAWASA, Mwanza, Arusha, Mtwara, Musoma, Tabora, Bukoba na Kigoma zina deni kubwa la tozo linalozidi shilingi milioni 300; na

iii. Mamlaka saba za maji za Mugango-Kiabakari, Wanging'ombe, Bunda, Itumba-Isongole, Kyela-Kasumulu, Tunduru na Busega hazikuwasilisha kabisa tozo hiyo.

## 2.15 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, wakati wa ukaguzi na ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na majitaka katika mamlaka za maji, EWURA ilitoa maagizo mbalimbali kwa mamlaka za maji. Uchambuzi unaonesha kuwa utekelezaji wa maagizo hayo umefikia asilimia 73. EWURA inazitaka mamlaka za maji kuhakikisha zinatekeleza kikamilifu maagizo hayo ili kuboresha utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini.

## 2.16 Bodi za Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, jumla ya Mamlaka 74 kati ya 83 zilikuwa na Bodi za Wakurugenzi. Mamlaka 9 hazikuwa na Bodi za Wakurugenzi kutokana na sababu mbalimbali. Kukosekana kwa Bodi hizo kunadhoofisha usimamizi wa mamlaka husika na kuchelewesha utoaji wa maamuzi, hali inayopunguza ufanisi katika utoaji wa huduma. Mamlaka za maji ambazo hazikuwa na bodi ni DAWASA, Musoma, Mugango-Kiabakari, Igunga, Kasulu, Mwanhuzi, Namanyere, Utete, na Kakonko.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UPIMAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

### 3.1 Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Maji

Mwongozo wa EWURA wa Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022, umeelekeza namna ya kupima utendaji wa mamlaka za maji. Katika Mwongozo huo, mamlaka za maji zinapimwa kwa kushindanishwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000. Kundi la pili ni mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na kundi la tatu ni mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000. Katika makundi hayo, mamlaka za maji zilipimwa katika makundi mawili ambayo ni;

i. Upimaji wa Jumla ambao unaangalia namna ambavyo mamlaka ya maji imetekeleza viashiria vya kiutendaji, imefikia viwango vya huduma vinavyokubalika na imetekeleza masharti ya kiudhibiti *(Overall Ranking).*

ii. Upimaji kuangalia namna ambavyo mamlaka imetekeleza malengo iliyojiwekea katika mpango biashara wake *(Utility Ranking).*

### 3.2 Matokeo ya Upimaji

Matokeo ya utendaji wa jumla wa mamlaka za maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kulingana na vigezo vya upimaji, ni kama ifuatavyo:

**Kundi la I**

i. Mamlaka ya Maji Moshi iliibuka mshindi wa jumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 20 za kundi la kwanza. Aidha, Mamlaka ya Maji Rombo ilikuwa na utendaji wa chini zaidi katika katika kundi hili kwa kupata alama 44 ambayo ni wastani.

ii. Mamlaka ya Maji Iringa iliibuka mshindi katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati Mamlaka za Maji DAWASA na KASHWASA zikiwa na utendaji wa chini zaidi kwa kupata alama 0.

**Kundi la II**

i. Mamlaka ya Maji Nzega iliibuka mshindi wa jumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 28 za kundi la kwanza.

Aidha, Mamlaka ya Maji HTM ilikuwa na utendaji wa chini zaidi katika katika kundi hili kwa kupata alama 41 ambayo ni wastani.

ii. Mamlaka ya Maji Nzega iliibuka mshindi katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati Mamlaka za Maji HTM, Mtwara, Bunda, Maswa, Sengerema, Kondoa, Chato, Bariadi, Same-Mwanga na Busega zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao kwa kupata alama 0.

**Kundi la III**

i. Mamlaka ya Maji Biharamulo ilikuwa mshindi wa jumla ikiwa na alama 72 katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 35 za kundi la tatu, inayotafsiriwa kama vizuri sana, wakati Mamlaka ya Maji Liwale ikiwa na utendaji wa chini zaidi kwa alama 37 katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira, ambayo hairidhishi.

ii. Mamlaka ya Maji Utete iliikuwa bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea kwenye mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji za Mugango-Kiabakari, Chunya, Itumba-Isongole, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Kiomboi, Kyela-Kasumulu, Liwale, Mwanhuzi, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Tunduru, Ushirombo, Tunduma, Mkwajuni na Kakonko zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi kwa kupata alama 0.

Ikilinganishwa na miaka iliyopita, utendaji wa jumla wa Mamlaka za Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 unaonesha kuimarika zaidi kutokana na ongezeko la mamlaka za maji zenye utendaji unaoanzia vizuri hadi bora zaidi. Ulinganishi wa utendaji wa mamlaka za maji ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji kwa makundi yote matatu yameainishwa katika jedwali Na. 3-5.

**Jedwali Na.2 Ulinganishi wa utendaji wa jumla wa Mamlaka za Maji**

| Mwaka wa Fedha | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** |
|---|---|---|---|
| Idadi ya Mamlaka Zilizoshindanishwa | 83 | 82 | 83 |
| Utendaji wa Jumla (kwa asilimia) | | | |
| Bora zaidi | 0 | 1 | 5 |
| Vizuri sana | 13 | 20 | 11 |
| Vizuri | 33 | 38 | 46 |
| Wastani | 46 | 39 | 35 |
| Usioridhisha | 8 | 2 | 3 |

## Jedwali Na 3: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la I

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) |
| 1 | Arusha | 43.4 | 32.3 | 75.7 | B | Vizuri Sana | 5 | 55.5 | C | Vizuri | 7 |
| 2 | Dodoma | 41.5 | 33.5 | 75.0 | B | Vizuri Sana | 7 | 48.1 | D | Wastani | 10 |
| 3 | Iringa | 49.6 | 38.0 | 87.6 | A | Bora Zaidi | 3 | 79.7 | B | Vizuri Sana | 1 |
| 4 | Mbeya | 47.1 | 25.2 | 72.3 | B | Vizuri Sana | 8 | 71.2 | B | Vizuri Sana | 4 |
| 5 | Morogoro | 32.7 | 29.5 | 62.2 | C | Vizuri | 17 | 46.7 | D | Wastani | 11 |
| 6 | Moshi | 53.4 | 37.3 | 90.7 | A | Bora Zaidi | 1 | 78.2 | B | Vizuri Sana | 2 |
| 7 | Musoma | 28.0 | 28.0 | 56.0 | C | Vizuri | 19 | 4.0 | E | Usioridhisha | 18 |
| 8 | Mwanza | 39.4 | 29.3 | 68.7 | C | Vizuri | 12 | 48.1 | D | Wastani | 9 |
| 9 | Shinyanga | 38.3 | 33.2 | 71.6 | B | Vizuri Sana | 9 | 52.2 | D | Wastani | 8 |
| 10 | Songea | 52.4 | 36.9 | 89.3 | A | Bora Zaidi | 2 | 68.7 | C | Vizuri | 6 |
| 11 | Tabora | 34.0 | 28.3 | 62.3 | C | Vizuri | 16 | 39.7 | E | Usioridhisha | 14 |
| 12 | Tanga | 43.4 | 31.9 | 75.3 | B | Vizuri Sana | 6 | 44.0 | D | Wastani | 13 |
| 13 | Bukoba | 33.2 | 29.4 | 62.7 | C | Vizuri | 15 | 38.7 | E | Usioridhisha | 16 |
| 14 | Kigoma | 37.0 | 20.0 | 57.0 | C | Vizuri | 18 | 44.3 | D | Wastani | 12 |
| 15 | Babati | 43.5 | 35.1 | 78.6 | B | Vizuri Sana | 4 | 74.4 | B | Vizuri Sana | 3 |
| 16 | Kahama | 36.2 | 33.4 | 69.6 | C | Vizuri | 11 | 69.5 | C | Vizuri | 5 |
| 17 | DAWASA | 40.3 | 30.2 | 70.5 | B | Vizuri Sana | 10 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 18 | KASHWASA | 35.7 | 28.2 | 63.9 | C | Vizuri | 14 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 19 | Singida | 38.5 | 25.5 | 64.1 | C | Vizuri | 13 | 39.0 | E | Usioridhisha | 15 |
| 20 | Rombo | 23.3 | 21.5 | 44.8 | D | Wastani | 20 | 38.5 | E | Usioridhisha | 17 |

## Jedwali Na. 4: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la II

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) |
| 1 | Mtwara | 35.1 | 19.8 | 54.9 | D | Wastani | 19 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 2 | HTM | 20.2 | 13.3 | 33.5 | E | Usioridhisha | 28 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 3 | Sumbawanga | 36.3 | 22.2 | 58.4 | C | Vizuri | 18 | 18.2 | E | Usioridhisha | 18 |
| 4 | Lindi | 34.5 | 25.4 | 59.9 | C | Vizuri | 17 | 30.8 | E | Usioridhisha | 14 |
| 5 | Geita | 35.4 | 33.1 | 68.5 | C | Vizuri | 3 | 42.8 | D | Wastani | 9 |
| 6 | Mpanda | 34.2 | 27.9 | 62.1 | C | Vizuri | 14 | 38.7 | E | Usioridhisha | 11 |
| 7 | Njombe | 39.1 | 27.9 | 67.0 | C | Vizuri | 6 | 47.2 | D | Wastani | 6 |
| 8 | MANAWASA | 38.0 | 25.2 | 63.2 | C | Vizuri | 10 | 45.4 | D | Wastani | 7 |
| 9 | Wanging'ombe | 26.8 | 16.6 | 43.4 | D | Wastani | 26 | 35.9 | E | Usioridhisha | 12 |
| 10 | Bunda | 40.1 | 24.8 | 64.8 | C | Vizuri | 8 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 11 | Igunga | 45.4 | 36.7 | 82.1 | B | Vizuri Sana | 2 | 65.3 | C | Vizuri | 2 |
| 12 | Karatu | 37.1 | 26.8 | 63.9 | C | Vizuri | 9 | 47.3 | D | Wastani | 5 |
| 13 | Maswa | 37.0 | 24.1 | 61.1 | C | Vizuri | 15 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 14 | Nzega | 48.8 | 38.8 | 87.6 | A | Bora Zaidi | 1 | 69.0 | C | Vizuri | 1 |
| 15 | Sengerema | 35.6 | 15.7 | 51.3 | D | Wastani | 23 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 16 | Tukuyu | 31.1 | 18.8 | 49.9 | D | Wastani | 24 | 28.9 | E | Usioridhisha | 15 |
| 17 | Makambako | 40.6 | 22.0 | 62.6 | C | Vizuri | 13 | 57.7 | C | Vizuri | 3 |
| 18 | Mbinga | 31.7 | 22.3 | 53.9 | D | Wastani | 20 | 22.6 | E | Usioridhisha | 17 |
| 19 | Kasulu | 28.1 | 23.5 | 51.6 | D | Wastani | 21 | 40.2 | D | Wastani | 10 |
| 20 | Kondoa | 27.7 | 15.2 | 42.9 | D | Wastani | 27 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 21 | Chato | 33.2 | 18.2 | 51.4 | D | Wastani | 22 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 22 | Bariadi | 31.9 | 30.8 | 62.8 | C | Vizuri | 12 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) |
| 23 | Mafinga | 36.9 | 24.2 | 61.1 | C | Vizuri | 16 | 23.7 | E | Usioridhisha | 16 |
| 24 | Makonde | 32.5 | 30.3 | 62.8 | C | Vizuri | 11 | 44.7 | D | Wastani | 8 |
| 25 | Manyoni | 39.6 | 27.2 | 66.8 | C | Vizuri | 7 | 34.0 | E | Usioridhisha | 13 |
| 26 | Same-Mwanga | 29.7 | 19.8 | 49.5 | D | Wastani | 25 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 27 | Turiani | 39.0 | 28.3 | 67.4 | C | Vizuri | 4 | 48.0 | D | Wastani | 4 |
| 28 | Busega | 38.7 | 28.4 | 67.1 | C | Vizuri | 5 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |

## Jedwali Na. 5: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la III

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) |
| 1 | Vwawa-Mlowo | 31.9 | 21.6 | 53.6 | D | Wastani | 17 | 33.5 | E | Usioridhisha | 10 |
| 2 | Mugango-Kiabakari | 26.7 | 15.8 | 42.5 | D | Wastani | 30 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 3 | Biharamulo | 41.1 | 31.5 | 72.7 | B | Vizuri Sana | 1 | 30.8 | E | Usioridhisha | 12 |
| 4 | Chunya | 30.9 | 13.7 | 44.6 | D | Wastani | 27 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 5 | Gairo | 22.8 | 25.0 | 47.8 | D | Wastani | 23 | 24.0 | E | Usioridhisha | 16 |
| 7 | Ifakara | 32.1 | 20.2 | 52.3 | D | Wastani | 19 | 21.9 | E | Usioridhisha | 17 |
| 8 | Itumba-Isongole | 28.7 | 13.7 | 42.4 | D | Wastani | 31 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 9 | Kibaya | 36.3 | 20.3 | 56.5 | C | Vizuri | 12 | 41.0 | D | Wastani | 7 |
| 10 | Kibondo | 39.2 | 27.0 | 66.2 | C | Vizuri | 3 | 52.3 | D | Wastani | 3 |
| 11 | Kilindoni | 24.1 | 17.8 | 41.9 | D | Wastani | 32 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 12 | Kilwa Masoko | 36.2 | 20.2 | 56.4 | C | Vizuri | 13 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 13 | Kiomboi | 30.6 | 14.8 | 45.4 | D | Wastani | 26 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 14 | Kishapu | 37.2 | 23.2 | 60.4 | C | Vizuri | 9 | 33.2 | E | Usioridhisha | 11 |
| 15 | Kyela-Kasumulu | 26.8 | 12.2 | 38.9 | E | Usioridhisha | 34 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 16 | Liwale | 22.2 | 15.0 | 37.2 | E | Usioridhisha | 35 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 17 | Loliondo | 42.2 | 23.6 | 65.8 | C | Vizuri | 4 | 60.2 | C | Vizuri | 2 |
| 18 | Ludewa | 32.4 | 25.4 | 57.7 | C | Vizuri | 11 | 28.3 | E | Usioridhisha | 13 |
| 19 | Lushoto | 35.8 | 22.2 | 58.0 | C | Vizuri | 10 | 24.4 | E | Usioridhisha | 15 |
| 20 | Makete | 29.7 | 19.7 | 49.4 | D | Wastani | 22 | 15.2 | E | Usioridhisha | 18 |
| 21 | Mbulu | 35.9 | 27.5 | 63.4 | C | Vizuri | 7 | 36.7 | E | Usioridhisha | 8 |

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2024/25) |
| 22 | Mpwapwa | 40.8 | 27.2 | 68.1 | C | Vizuri | 2 | 51.6 | D | Wastani | 4 |
| 23 | Mwanhuzi | 31.0 | 16.1 | 47.2 | D | Wastani | 24 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 24 | Namanyere | 30.3 | 13.2 | 43.5 | D | Wastani | 29 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 25 | Namtumbo | 35.2 | 17.4 | 52.6 | D | Wastani | 18 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 26 | Ngara | 36.5 | 29.1 | 65.6 | C | Vizuri | 5 | 43.5 | D | Wastani | 6 |
| 27 | Ruangwa | 33.3 | 20.7 | 54.0 | D | Wastani | 15 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 28 | Rujewa | 32.4 | 22.8 | 55.2 | C | Vizuri | 14 | 25.1 | E | Usioridhisha | 14 |
| 29 | Songe | 31.1 | 19.8 | 50.9 | D | Wastani | 21 | 36.3 | E | Usioridhisha | 9 |
| 30 | Tunduru | 29.0 | 15.2 | 44.2 | D | Wastani | 28 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 31 | Ushirombo | 32.8 | 20.7 | 53.6 | D | Wastani | 16 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 32 | Utete | 37.2 | 26.5 | 63.7 | C | Vizuri | 6 | 66.2 | C | Vizuri | 1 |
| 33 | Maganzo | 40.9 | 21.4 | 62.3 | C | Vizuri | 8 | 50.6 | D | Wastani | 5 |
| 34 | Tunduma | 28.5 | 22.8 | 51.3 | D | Wastani | 20 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 35 | Mkwajuni | 29.2 | 18.0 | 47.1 | D | Wastani | 25 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |
| 41 | Kakonko | 27.7 | 12.5 | 40.2 | D | Wastani | 33 | 0.0 | E | Usioridhisha | 19 |

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO

Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, imebainisha uwepo wa changamoto mbalimbali zinazohitaji kuchukuliwa hatua za kuboresha. EWURA, kama taasisi ya udhibiti, imeandaa mapendekezo mahsusi yanayolenga kusaidia kufanikisha malengo ya kitaifa na kimataifa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za maji na usafi wa mazingira nchini. Jedwali Na. 6 linaonesha masuala hayo pamoja na mapendekezo ya hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa ili kuboresha na kuleta ufanisi katika Sekta ya Maji.

**Jedwali Na. 6: Masuala yaliyobainika na Mapendekezo**

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Huduma duni za usafi wa mazingira | Asilimia 71 ya mamlaka za maji hazina miundombinu ya kutibu majitaka na tope kinyesi, hivyo kumwaga/ kutiririsha majitaka hayo na topekinyesi kwa njia zisizo salama | Kufanya mapitio ya mipango ya biashara pamoja na bajeti za mwaka ili kujumuisha ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kupata maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi | Juni 2027 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kujenga miundombinu ya kutibu majitaka na tope kinyesi ili kupunguza pengo la uwezo wa kutibu majitaka na topekinyesi | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Asilimia 54 ya Mamlaka za Maji hazina magari ya kunyonya majitaka na vifaa vya uondoaji topekinyesi | Kutafuta rasilimali fedha, ikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uwekezaji wa kuondoa na kusafirisha majitaka na topekinyesi | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |
| | | Wastani wa uzingatiaji wa ubora wa majitaka kwa mahitaji ya oksijeni kibiolojia (BOD) na kikemikali (COD) ulikuwa ni asilimia 43 ambayo ni chini ya kiwango cha huduma cha asilimia 100 | Kutekeleza hatua za kuboresha ubora wa majitaka, ikiwemo kukarabati au kufanya matengenezo ya miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |
| 2 | Uzingatiaji mdogo wa klorini baki kwenye maji (Residual Chlorine) | Wastani wa uzingatiaji wa klorini baki kwenye maji yanayosambazwa na mamlaka za maji ulikuwa asilimia 27, ambayo ni chini ya kiwango kinachotakiwa cha asilimia 100 | Kuhakikisha wataalamu wenye sifa stahiki wanaajiriwa na wanahusika katika kutibu maji na kufuatilia ubora wake | Juni 2027 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kutibu maji na matumizi sahihi ya dozi kwa mujibu wa Mwongozo wa utaratibu wa kutibu maji | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Kiwango kikubwa cha Upotevu wa Maji | Wastani wa upotevu wa maji ulikuwa asilimia 42, ambayo ni juu ya kiwango cha huduma kinachokubalika cha chini ya asilimia 20 | Kuandaa mikakati ya kupunguza upotevu wa maji kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kuhakikisha uchaguzi, ufungaji, upimaji na matengenezo sahihi ya mita za maji kwa mujibu wa Miongozo ya EWURA | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |
| 4 | Uwiano mdogo waa uzalishaji wa maji dhidi ya mahitaji | Wastani wa uwiano wa uzalishaji ulikidhi asilimia 52 tu ya mahitaji, hivyo kupelekea uwepo wa mgao wa maji | Kuendeleza vyanzo vya ziada/mbadala vya maji | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |
| | | | Kutekeleza hatua za kuimarisha uimara wa miundombinu dhidi ya athari za tabianchi | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |
| | | | Kupanua miundombinu ya uzalishaji na usambazaji w maji na kuongeza uunganishaji wa wateja | Kulingana na mipango ya biashara ya Mamlaka za Maji | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza upatikanaji wa maji, ikiwemo Gridi ya Maji ya Taifa na ujenzi wa mabwawa | Juni 2030 | Wizara ya Maji |
| | | | Kutafuta rasilimali fedha ikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi, hati fungani (green bonds, mifumo ya ufadhili mchanganyiko (blended financing), ufadhili unaozingatia matokeo (results-based financing), pamoja na mbinu nyingine bunifu za utafutaji wa fedha. | Juni 2027 | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Urejeshaji usioridhisha wa gharama za uendeshaji | Wastani wa uwiano wa uendeshaji (working ratio) wa mamlaka za maji ulikuwa 1.3 na uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu wa miundombinu dhidi ya mapato (operating ratio) ulikuwa 1.95 ambayo ni juu ya viwango vya huduma vinavyokubalika vya 0.67 na 0.8 mtawalia, ikiashiria udhaifu katika kumudu gharama za uendeshaji | Kutekeleza mikakati ya kuboresha utendaji wa kifedha, kwa kuzingatia ufanisi wa kiutendaji na kuongeza mapato. Hatua za kipaumbele ni pamoja na kupunguza upotevu | Juni 2027 | Mamlaka za Maji |
| | | | Kufanya mageuzi ya kimuundo kwa kuzingatia hasa kuunganisha mamlaka ndogo na dhaifu kifedha kuwa taasisi kubwa na zenye ufanisi wa kibiashara (*clustering*), ili kuimarisha urejeshaji wa gharama, na kuhakikisha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira. | | |
| 6 | Bei za maji zilizopitwa na wakati na zisizoendana na gharama halisi za uendeshaji | Mamlaka za maji kuendelea kutumia bei zisizowezesha kurejesha gharama za uendeshaji | Maandalizi ya mipango ya biashara inayoakisi gharama halisi za uendeshaji zitakazojumuishwa kwenye marekebisho ya bei mpya za maji yapewe kipaumbele. | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 imeonesha uwepo wa maendeleo ya utendaji wa mamlaka za maji. Pamoja na mafanikio hayo, changamoto zilizobainika zinatoa fursa ya kujifunza na kubuni mbinu mpya za kuboresha utendaji, kuongeza uwajibikaji, na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa wananchi. Ili kufikia malengo ya upatikanaji wa huduma za majisafi na salama na mazingira safi, kunahitajika jitihada za pamoja, matumizi sahihi ya teknolojia, na ushirikiano wa karibu kati ya EWURA, mamlaka za maji, Serikali, na wadau mbalimbali.

Inatarajiwa kwamba utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii utachochea maboresho makubwa katika sekta ya maji na usafi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma zenye ubora, kupunguza changamoto za miundombinu, na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji. Hii itasaidia kujenga sekta yenye uwezo wa kujitegemea, inayojibu mahitaji ya jamii kwa wakati na kwa ufanisi.

EWURA itaendelea kutekeleza majukumu yake ya udhibiti kwa weledi na uwazi, na kuishauri Serikali kuhusu sera, sheria, na kanuni zitakazowezesha ukuaji endelevu wa sekta ya maji na usafi wa mazingira. Aidha, itaendeleza ufuatiliaji wa karibu wa mamlaka za maji ili kuhakikisha zinafanya kazi kwa viwango bora, zikilenga kutoa huduma jumuishi, salama, na nafuu kwa wananchi wote.

Kwa pamoja, juhudi za wadau wote katika sekta hii zitaleta mabadiliko chanya na kudumisha maendeleo endelevu ya huduma za maji na usafi wa mazingira, msingi muhimu kwa ustawi wa kijamii, afya ya umma, na maendeleo ya kiuchumi ya taifa.

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

MAKAO MAKUU YA EWURA
Jengo la EWURA, Mtaa wa EWURA
3 Mtaa wa EWURA,
4114 Tambukareli,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz
Tovuti https://www.ewura.go.tz
Huduma kwa Wateja: 0800110030

ewuratanzania ewuratanzania ewuratanzania EWURA TV